

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA PILI

KIKAO CHA TATU

04 FEBRUARI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA PILI

KIKAO CHA TATU – TAREHE 04 FEBRUARI, 2021

I. DUA:

II. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

III. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

31. MHESHIMIWA ANNA RICHARD LUPEMBE (NSIMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatengeneza barabara za Kata ya Katumba.

32. MHESHIMIWA KUNTI YUSSUF MAJALA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-


Je, ni lini Serikali itapeleka Walimu wa kike katika Shule za Msingi Birise na Donsee ambazo hazina Walimu wa kike.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

33. MHESHIMIWA SOUD MOHAMMED JUMAH (DONGE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, ni fedha kiasi gani Tanzania imeomba na kupewa kutoka katika Mfuko wa Fedha za kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi wa Umoja wa Mataifa.



WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

34. MHESHIMIWA HASSAN SELEMAN MTENGA (MTWARA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali haioni sababu kwa sasa kutumia Bandari ya Mtwara kusafirisha Korosho zinazolimwa Kusini badala ya kutumia njia ya magari ambayo inasababisha uharibifu mkubwa wa barabara kwenda Bandari ya Dar es Salaam.

**35. MHESHIMIWA NASHON WILLIAM
BIDYANGUZE (KIGOMA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga daraja katika Mto Malagarasi Ilagala.

WIZARA YA MAJI:

**36. MHESHIMIWA ALLY ANYIGULILE MLAGHILA
(KYELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Suluhisho la tatizo la maji katika Wilaya ya Kyela ni kutumia chanzo cha Ziwa Nyasa kama ilivyoelezwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020:-

Je, ni lini sasa mradi huo utanza kutekelezwa.

**37. MHESHIMIWA FLORENT LAURENT
KYOMBO (NKENGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Kata za Gera, Ishozi, Ishunju, Kanyigo, Kashenye, Bwanjai, Bugandika, Kitobo, Buyango na Ruzinga katika Jimbo la Nkenge zina shida kubwa ya maji licha ya kwamba zipo kwenye mwambao wa Ziwa Victoria: -

Je, ni lini Serikali itawafikishia Wananchi wa Kata hizo maji kutoka Ziwa Victoria kama inavyofanya kwa Mikoa mingine inayopata maji kutoka katika Ziwa hilo.

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

38. MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESHER KABATI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, ni lini Serikali itaipatia Hospitali ya Mkoa wa Iringa mashine ya CT-SCAN.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

39. MHESHIMIWA DKT. STEPHEN LEMOMO KIRUSWA (LONGIDO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, ni fedha kiasi gani zimepatikana katika operesheni ya kudhibiti utoroshaji wa mifugo nje ya nchi na fedha hizo zimetumikaje.

**40. MHESHIMIWA ANGELINA ADAM
MALEMBEKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:- Kuna mpango wa kujenga bandari kubwa ya uvuvi inayotegemewa kutoa ajira zipatazo 30,000:-

Je, ajira kwa upande wa Zanzibar zitakuwa ngapi kati ya hizo.

WAZIRI WA NISHATI:

**41. MHESHIMIWA JOSEPH MICHAEL MKUNDI
(UKEREWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Pamoja na kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya kusambaza umeme Vijijini kupitia mradi wa REA bado kuna shida kubwa katika maeneo ya Vitongoji kwenye Vijiji hivyo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kuwa umeme unasogezwa kwenye maeneo ya Vitongoji ambavyo bado havijapata huduma hiyo.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI MKUU:

Kwamba, Bunge sasa lijadili Hotuba ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyoitoa wakati wa Ufunguzi wa Bunge la Kumi na Mbili tarehe 13 Novemba, 2020.

(Majadiliano yanaendelea)



**DODOMA
04 FEBRUARI, 2021**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**